TANGAZO LA SERIKALI NA. 220 la Tarehe 28/3/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetenenezwa chini ya kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA HIFADHI YA MISITU NA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 265 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Misitu na Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Misitu na Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kuongeza tafsiri ya msamiati mpya kulingana na mtiririko wa kialfabeti kama ifuatavyo:

Sura ya 184

""mifugo" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifungo;".

Marekebisho ya kanuni ya 6

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 6(1) kwa kuongeza maneno "isipokuwa kwa kufuata kanuni za kilimo" mara baada ya neno "mazingira".

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza na Jedwali la Pili

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza na Jedwali la Pili kwa kufuta neno "DBH".

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*